
Jarida La Kila Mwezi

# NGURUMO ya Mwandishi

Toleo La XVII
Februari MMXXIII



## USIBAKI NYUMA...

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— Usibaki Nyuma…—Uk 02

**MWANDISHI WETU**— Clarency Sanga— Uk 03

**New In Town—** MPATANISHI, NDEGE TUNDUNI na HARUFU YA KIFO **-** 04

**PITIO LA VITABU**— MFADHILI— Uk 05

**MAKALA**— SAIKOLOJIA: Usijitotoshe —Uk 06 na 07

**RIWAYA:** Nilimuua Dada Niolewe Na Shemeji — uk 08 na 09

**MIAMBA WA AFRIKA:** Samora Machel (01) — Uk 10

**ANA KWA ANA**: Zamira Sanguti: Mahusiano yake na vitabu -Uk 11

**RIWAYA:** Mpigambio—Uk 12 na 13

**SHUBAKA LA VITABU—** Na. Selina Banzi **-**Uk 14

**KITABU NILICHOSOMA:** Kovu la Moyo — Uk 16

**MATANGAZO:** Uk 17

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**MHARIRI: RICHARD MWAMBE**
**MSAIDIZI: REY STANLEY**

**WASILIANA NASI**

**0766 974 865 AU 0672 160 016**

**WhatsApp: +255 734 550 514**

## TAHARIRI: Usibaki Nyuma!

Wasalaam ninyi nyote Tanzania na nje yake,

Kwanza kabisa nikutakeni radhi kwa kuwa toleo letu hili limechelewa kukujieni. Lakini yote haya yamesababishwa na vifaa vyetu kupata mushkeri hivyo kushindwa kuandaa jarida kwa wakati. Lakini naamini sasa kuwa, kwa nguvu za Mwenyezi Mungu tutaendelea vyema kwa utaratibu uleule wa mwanzo.

Kwanza nimshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai. Nakushukuruni ninyi pia ambao mlinitumia 'ya soda' wakati ule wa kumbukumbu ya mazazi yangu hapo Februari 15. asanteni na Mungu akujaalieni heri yote!

Pili napenda kukujuzeni kuwa vitabu vyetu pendwa vya riwaya za kijasusi na upelelezi vya MPATANISHI na HARUFU YA KIFO tayari vimerudi madukani. Hivyo kama wewe ulikuwa bado kupata nakala hizo, wahi sasa uzipate. Na pia kile kitabu chetu cha CRONOC 7 nacho kipo mbioni kuingia dukani. Hivyo ladha iliyo kamili imekujia.

Zaidi ya hapo pia Jamvi la Simulizi katika kuadhimisha miaka kumi, tumepanga kuwapa zawadi nyingi tu ninyi wasomaji wetu maana kama si ninyi basi tusingekuwa hapa.

Lakini moja ambalo ningependa kuwadokezea ni kuwa tunaandaa pikniki ya Bagamoyo na gaharama zote za usafiri na vinywaji ni juu ya Jamvi la Simulizi, wewe utatakiwa kuandaa chakula chako tu. Hii tutaitangaza mapema mwezi wa nne. Na kutakuwa na limited seats. Yaani watu 20 tu maalum kwa wakazi wa Dar es salaam na pembezoni.

Kwanini tunafanya hivi? Ni kurudisha shukrani kwa wasomaji wetu mnaotupenda sana. Lakini ili kupata hizo nafasi kutakua na QUIZ ndogo tu ili mtu apate nafasi kwa haki na si upendeleo. Zaidi ya hapo kutakuwa na zawadi nyingine kem kem kwa ajili yako wewe na yeye na Yule. Cha msingi tu ni kuwa wewe uwe mshabiki wa kazi za Jamvi la Simulizi.

Basi upatapo jarida hili, tafadhali mtumie na mwenzio kwa whatsapp au email au vyovyote vile ili naye aburudike na kupata habari hii.

Habari nyingine nyingi zitakuwa katika App yetu ya Jamvi la Simulizi, kama bado hujaipakua, unapitwa na mengi, ipakue sasa. Kama hujui jinsi ya kupakua App hiyo, soma ukurasa wa mwisho wa jarida hili.

Richard Mwambe
Iringa-Mawelewele
10 March, 2023

# MWANDISHI WETU: CLARENCY SANGA

**Hii ni safu maridhawa inayokukutanisha wewe msomaji na mwandishi unayempenda. Katika toleo hili tunakuletea mwandishi machachari anayesumbua kwa sasa katika tasnia hii ya uandishi wa riwaya. Huyu hapa…**

Jina langu kamili naitwa Shukrani Said Sanga, kwenye tasnia ya uandishi nafahamika kama Clarency Sanga. Nimezaliwa katikati mwa miaka ya 90. Au naweza kusema nimezaliwa 94's huko Songwe katika mji mdogo wa Mlowo. Kwa sasa nipo Sumbawanga kwenye utafutaji.


Nimesoma japo sio kwa elimu kubwa sana. Kabla sijawa mwandishi, nilikuwa msomaji wa riwaya kisha nikapenda kuandika. Nikajaribu nikaweza kuandika japo bado sijafika kiwango ninachokitaka.

Nimeanza rasmi kuandika mwaka 2019/2020. Shukran zangu za dhati ziende kwa Hammie Rajabu na Kijogoo kwa kuniwezesha kuchapa kitabu changu cha kwanza Nguvu ya Risasi.

Mpaka sasa nina zaidi ya riwaya 16, hapo ni jumla ya vitabu na *softy copy*. Baadhi ya riwaya ni kama; Ikishindkana, Kitubio, Moyo Uliopotea, Dosari, Mguu Ndani Mguu Nje, Tabasamu la Gaidi, Nusu Shari n.k

Uandishi wa vitabu umenipa marafiki wengi sana, pia umenipa maadui, hata kama siwajui ila najua wapo. Kikubwa uandishi naudai na utanilipa.

Mpaka sasa riwaya nilizochapa kitabu zipo na ni hizi. NGUVU YA RISASI, NUSU SHARI, DOSARI, TABASAMU LA GAIDI, MOYO ULIOPOTEA, IKISHINDIKANA (achaneni na mwili wake, rudini na moyo wake), MGUU NJE MGUU NDANI (karibu mchezoni).



Mimi ninawahusudu waandishi wote, nasoma riwaya za wote sichagui na nawapenda wote. Na hii ni kwa sababu wote ni waandishi pendwa kwangu.

Ukishakuwa mwandishi basi ushakuwa mwandishi pendwa kwangu. Sibagui sichagui.

Kuhusu soko la vitabu, kweli mbisha wengi ni mchawi, na mimi nasema kama wao, ni gumu kweli kweli na ukija uje umejipanga kweli kweli.

Mtu akihitaji kazi zangu anaweza kuwasiliana na mimi kwa nambari za simu 0742449173 au Facebook natumia Clarency Sanga. Pia kwa Suleiman kijogoo anaweza akavipata.

Kwa wasomaji napenda kuwaambia kituo kinachofuata ni KIKI, pamoja na mfululizo wa riwaya za Kelvin Kamba.

Penda kusoma vitabu

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Faida za kusoma vitabu:

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Huboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Huboresha Mtazamo na Umakini

Neno langu kwa waandishi ni kwamba UWANDISHI UHESHIMIWE.
neno kwa wote wakumbuke....

"Katikati ya Jana na kesho ndio penye muda wa kutimiza malengo yako"
Asante.

**Ngurumo ya Mwandishi tunakutakia heri na Baraka katika uandishi wako.**

## New In Town!

### MPATANISHI
©Richard Mwambe


Mpatanishi ni kitabu cha riwaya kilichoshika sana hisia za watu miaka mitatu nyuma. Kitabu hiki kilichoandikwa na Richard Mwambe kinasimulia kisa cha kusisimua cha kipelelezi.
Katika kisa hiki, Kamanda Amata anafanya upelelezi juu ya tetesi iliyopo kwamba makaburu wa Afrika Kusini wamewateka na kuwahifadhi majasusi wa Kitanzania katika magereza yao. Wakati huohuo Makaburu nao wanadai kuwa serikali ya Tanzania imewashikilia majasusi wa kikaburu katika magereza yao.

Katika mgogoro huo, ndipo inaundwa tume ya upatanishi kati ya makundi haya mawili.

Lakini ukweli wa hilo upoje?

Ukiwasiliana na mwandishi Richard Mwambe atakuelekeza jinsi ya kukipata kitabu hicho na kitakufikia popote ulipo.

**Simu: 0766974865**




### NDEGE TUNDUNI
©Japhet Nyang'oro Sudi

Kinasimulia nini?
Mkasa unaanza pale ambapo dakika 30 kabla ya tukio la kupigwa risasi Spika wa Bunge, msichana mmoja anaandika facebook juu ya kutokea kwa tukio hilo, huku akitaja idadi ya risasi alizopigwa Spika.
Tukio lilipotokea, posti yake ikajizolea umaarufu mkubwa mitandaoni. Wengi walijiuliza msichana huyo alijujaje kuwa Spika angepigwa risasi, tena risasi tatu!?
Harakati za kutafuta wahusika wa mauaji zilipoanza, vyombo vya usalama havikuchelewa kumpata msichana huyo.

Anapokamatwa tu msichana anawaambia wanausalama kuwa amebakiza muda wa saa tatu na nusu tu za kuishi, hivyo wamuulize maswali ya msingi. Saa tatu na nusu zinapomalizika, linatokea tukio la kushangaza, ambalo linafanya waliomhoji waambulie kubaki na ujumbe mzito wenye utata mwingi.
Ujumbe unaowafanya wabobezi wa masuala ya usalam wanong'onezane kuwa NDEGE TUNDUNI, adui kajileta mwenyewe kwenye kifo chake. Ni riwaya nzuri ya kijasusi na kipelelezi, iliyoandikwa kwa ustadi mkubwa.
Kama wewe ni mpenzi wa riwaya, usiache kusoma kitabu hiki.

Kitabu hiki kipo nchi nzima… wasiliana na mwandishi.

**Simu: 0762204166**

### HARUFU YA KIFO
**©Richard Mwambe**

Hii ni Harufu ya Kifo, kitabu chenye simulizi pendwa kabisa ya kipelelezi na ujasusi.

Ugonjwa unaoua Waafrika kila uchao unapatiwa chanjo kutoka kwa wanasayansi wa Kitanzania waliojificha kwenye maabara kubwa na ya kisasa huko katikati ya Msitu wa Londo, Mkoani Lindi.
Kwa kudai kwamba chanjo hiyo haina vigezo kutumika kwa binadamu, WHO wanakuja na kuchukua sampuli pamoja na kanuni ya jinsi ilivyotengenezwa wakisema kwamba wanaipeleka Geneva kwa uchunguzi ili kuona ubora wake kabla ya matumizi. Lahaula lakwata! Dakika kumi hivi tangu ile ndege iruke pale Lindi, inalipuka vibaya. Na muda huohuo ile maabara kule msituni inateketea kwa moto. Mshangao!

Madam S anamwambia Amata "rudi ukafanye uchunguzi" jambo limezua jambo.
Je nini kipo nyuma ya milipuko hiyo?

Wasiliana na mwandishi Richard Mwambe upate nakala yako.

**Simu: 0766974865**

**Hakikisha unajipatia nakala laini za jarida lako la kifasihi nchini. Kila mwezi jarid hili linakujia tarehe 5;**

**Utalipataje? Wasiliana na wasambazaji wetu kama ifuatavyo, mawasiliano yote kwa WhatsApp**

**NGURUMO : +255 766974865, 0672160016**

# KITABU: MFADHILI

**Katika safu ya Pitio La Vitabu, leo tunaipitia riwaya ya MFADHILI iliyoandikwa na Hussein Issa Tuwa, na imepata cheti cha ithibati na kutumika mkwenye mtaala wa elimu ya sekondari.**

**Tahakiki hii inaletwa kwenu na Mwl. Furaha Venance**

## Utangulizi kuhusu Riwaya.

Mfadhili ni riwaya iliyoandikwa na Hussein Tuwa, ni riwaya inayoongelea juu ya penzi zito baina ya watu wawili, Gaddi Bullah na Dania Theobald na jinsi ambavyo penzi hilo linavyoingiliwa na mitihani, majaribu na misukosuko mikubwa na namna ambavyo kila mmoja anavyojaribu kukabiliana na hiyo misukosuko. Ni riwaya inayogusa moyo na isiyochosha kusomwa na wasomaji wa kila aina.

Mwandishi Hussein Tuwa pamoja na kuandika riwaya hii, pia ameandika riwaya nyingine inayoitwa, Mkimbizi.

## WAHUSIKA

Wahusika ni wakala wa vitendo katika kazi ya fasihi. Wahusika ni watu au viumbe waliokusudiwa na mwandishi wawakilishe tabia za watu katika kazi ya fasihi. Na wahusika katika kazi ya fasihi ni Muhusika/wahusika wakuu na wahusika wasaidizi.

### Wahusika wakuu.

Hawa ni wahusika wanaojitokeza mara kwa mara katika kazi ya fasihi na mara nyingi ndio wanaobeba dhamira kuu ya mwandishi lakini pia husaidia kujenga dhamira ndogondogo. Riwaya hii ya Mfadhiri ina wahusika wakuu wawili, Gaddi Bullah na Dania.

**1. Gaddi Majid Bullah**

Ø Ni mtu mcheshi na mchangamfu, kama mwandishi anavyothibitisha anaposema, " Na hii ilitokana na jinsi Gaddi alivyobadilika mara baada ya kukutana na Dania na kurudia ucheshi na uchangamfu wake wa zamani" [Uk 97]

Ø Ni msomi aliyeajiliwa katika kampuni ya mawasiliano, mwandishi anathibitisha hili anaposema, "….kampuni ile kubwa ya mawasiliano nchini ambayo ilimwajiri mara baada ya kumaliza masomo yake ya elimu ya juu miaka mitano iliyopita." [Uk 57]

Ø Anashushwa cheo kutoka Meneja wa mkoa katika tawi la Arusha hadi kuwa Afisa wa kawaida wa kukusanya madeni. Rejea Ukurasa wa 57.


Ø Kaka pekee wa Bi Hanuna.

Ø Mume wa Nyambuja ambaye wanakuja kuvunja ndoa yao kutoka na kusalitiwa, kama mwandishi anavyothibitisha anaposema, "Wiki moja baadaye Gaddi na Nyambuja waliachana kisheria…." [Uk 68]

Ø Anasalitiwa na Mke wake kwa kuanzisha uhusiano na mwanaume mwingine, mwandishi anathibitisha hili kupitia muhusika Nyambuja anaposema katika barua aliyomwandikia Gaddi, "Gaddi nimependana na mtu mwingine, na nimekuwa nikisaliti ndoa yetu kwa muda mrefu." [Uk. 65]

Ø Hakufanikiwa kupata mtoto katika uhai wa ndoa yake na nyambuja, kama mwandishi anavyothibitisha hili anaposema, "Gaddi aliguna kwa mshangao, akilini mwake akikumbuka jinsi yeye alivyokuwa akisononeka kwa kutopata mtoto wakati wa ndoa yake..." [Uk. 83]

## PITIO LA VITABU




www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Ø Anaanzisha uhusiono wa mapenzi na mwanamke mwingine aitwatae Dania

Anafaa kuigwa

2. **Dania Theobald.**

Ø Ni binti wa miaka kama ishirini na nne.

Ø Ni binti mrembo na wakuvutia.

Ø Ni binti anayetoka katika familia ya kitajiri, kama mwandishi anavyothibitisha akimtumia muhusika Mama Mlole anaposema, " Akiwa ni mtoto aliyetoka katika familia ya Kitajiri." [Uk. 81]

***ITAENDELEA...***

# USIJITOTOSHE ILA USIACHE KUWA MNYENYEKEVU



**Na: Neema Mgao**

Kwanza tuone maana ya maneno hayo mawili.

## Kujitotosha.

Hii ni ile hali ya kufanya mambo ya kitoto, ni ile hali ya kujiona hutoshi kwenye utekelezwaji wa jambo fulani. Waweza sema ni ile hali ambayo mtu hujionesha kuwa anaweza kufanya jambo fulani kwa uchache.

**Unyenyekevu.**

Ni ile hali ya kuwa na heshima, ile hali ya kujali au ile hali ya kunyenyekea kwa watu. Ieleweke kuwa kunyenyekea sio kujishusha au kujidharaulisha. Bali ni kuonesha heshima.

Baada ya kuona maana ya maneno hayo basi sasa tuone ufanyaji kazi wake.

Kujitotosha, mara ngapi umesikia mtu akisema "jamaa ana mambo ya kitoto", yawezekana ni mara nyingi, lakini hapa tunaongelea ile hali ya kujifanya mtoto wakati kiuhalisia sio kweli. Sasa unakuta mtu amechaguliwa kuongoza mahali, anadhani kuwa ili aonekane anafaa basi anaanza kujitotosha, yaani anaanza kufanya mambo kwa kujishusha saana, sasa watu wamekuamini wamekupa jukumu la kuwaongoza, sasa kuanza kujitotosha ndo ili iwe na maana ipi? Jiamini fanya kazi kwa ukubwa ulioaminiwa.

Wengine wanadhani unyenyekevu ni kujifanya haujui, hapana. Unyenyekevu ni kuwa na nidhamu ya hali ya juu sana katika ufanyaji kazi wako. Unyenyekevu ni kuheshimu kila lika katika maisha yako, unyenyekevu sio kujitotosha.

Unyenyekevu sio kuomba omba msamaha wakati haujakosea, jiamini kwa kazi unayoifanya, katika jambo unalofanya, jiamini na ujikabidhi kwa Mungu, panga namna nzuri itakayokuridhisha katika kutekeleza majukumu yako ya kila siki, ukishajiandaa na kupanga mikakati ya kuwezesha kufanikisha basi fanya sasa jambo hilo kwa weledi. Sasa katika kulifanya jambo hilo, maadamu umeshalipangilia vizuri basi usijitotoshe bali uwe na nidhamu.

Usijitotoshe, wewe ni mtu mkubwa, na ndio maana ukakabidhiwa jukumu hilo, sasa ukijifanya uoneshe kuwa huwezi si unaona utawavunja moyo waliokuamini na kuamini kuwa unaweza kulifanya jambo kwa weledi. Ukijitotosha unawapa kazi kwanza ya kukufanya ujione unaweza,  na unaweza ukawapa kuenda mbele zaidi ya wao kuhakikisha wanakufatilia kwenye utekelezaji wa majukumu yako.

Jiamini na jiaminishe katika shughuli zako, jiaminishe kwao kuwa wewe ni imara na unaweza kutekeleza majukumu yako bila usimamizi wala uangalizi wao. Watu wengi wanadhani kuwa ili wapendwe basi ni kujitotosha, yaani unakuta ni mtu mkubwa tuu lakini anafanya mambo ya hovyo hovyo tuu mpaka unaweza kudhani mtu ameruka hatua ya ukuaji. Jiamini wakikuamini, usijitotoshe. Unapojitotosha wanakudharau, utekelezwaji wa mambo mbalimbali unahitaji watu waliomakini ili kuimarisha mambo hayo, sasa ukijiweka kuwa wewe ni mtoto si unaona baadhi ya mambo yatakwama.jiamini fanya mambo kwa weledi na uzingativu.
Kisaikolojia, ile tabia unayoifanya mara kwa mara inakaa kichwani, sasa ikiwa unajidharau na kujitotosha basi utaonekana haufai, na ukizoea kujidharaulisha na unajidharau kweli na wanakudharau pia.

**Madhara ya kujitotosha.**

1. Hawatokuamini.

# -SAIKOLOJIA–
# FANYA MAAMUZI MAGUMU

Utaona wanakuona una mambo ya kitoto hivyo wanaweza wakakutoa katika nafasi uliyopo. Hawatokuamini tena, sasa watamwaminije mtu asiyejiamini yeye mwenyewe, mtu anaejitotosha yaani anajiona hatoshi mahali fulani, huyo ataaminikaje, ni wazi kwamba imani itaondoka.

**2. Hawatokuheshimu.**

Sio tuu wataacha kukuamini, lakini pia hata heshima itaondoka, sasa utamheshimu vipi mtu ambae yeye hajiheshimu. Hawatokuheshimu kwa kuwa mpaka wanakupa usimamizi wa jambo fulani wewe ni wazi kuwa wamekuona unafaa. Sasa ukishaonesha hali ya kujitotosha ni dhahiri kuwa watakudharau. Anaheshimiwa mtu anaejiheshimisha, yeye mwenyewe anajidharaulisha ataheshimiwaje, hivyo jua kabisa ukijitotosha hawatokuheshimu.

**3.Watakutoa nafasi uliyopo.**

Ndio, watakutoa katika nafasi waliyoamini unaweza kufanya jambo. Sasa yanini kumpa mtu heshima ambapo yeye mwenyewe anajitotosha. Yaani yeye anajiona kuwa ni mtoto kutekeleza mambo mbalimbali sasa ni lazima atafutwe mtu aliye na maamuzi thabiti katika kuendesha mambo mbali mbali. Watakutoa thamani katika utekelezaji wa mambo yako.

Usijifanye haujui mambo ingawa inakupasa kujinyenyekeza sana, unyenyekevu katika kazi zako za kila siku ni jambo muhimu. Ila nyenyekea pale inapopaswa kunyenyekea, sio muda wote hata muda unaoona hili jambo ni hatari kwako eti umesimamia tuu kunyenyekea, hapana. Uwe imara na katika kunyenyekea uwe mtu wa kujiamini. Dunia inataka mtu makini anaejiamini hivyo usiruhusu watu kujua madhaifu yako. Bali watu waushuhudie uhodari wako muda wote, watu wakuone imara nyakati zote, watu wanahitaji kiongozi anaejiamini sana ili kuwaongoza vyema, hivyo ni muhimu kujiamini, kuwa na maamuzi imara na kuwa na utashi wa kufikiri mambo mbali mbali yatakayoleta tija katika maisha yako ya kila siku.
Usijitotoshe.

Neema Mbilinyi Mgao.
WhatsApp no. 0746-139654.
Dodoma.

***unyenyekevu katika kazi zako za kila siku ni jambo muhimu.***

***Dunia inataka mtu makini anaejiamini hivyo usiruhusu watu kujua madhaifu yako.***

# HADITHI: NILIMUUA DADA NIOLEWE NA SHEMEJI-02



***Ilipoishia***

**Kila jioni ya siku za Jumatatu hadi Ijumaa, kijana yule alipita pale. Kila alipopita aliwakuta marafiki hawa wawili wakiwa katika mkao uleule.**

***Endelea…***

Wakati mwingine alimkuta dada peke yake. Hakuacha kuwasalimia kisha huchukua hamsini zake. Mazoea hujenga tabia, walisema watu wa zamani. Ndivyo ilivyokuwa. Mazoea ya kupita kila jioni yalimjengea kijana yule tabia. Ilikuwa lazima apitie. Alipowakuta alisimama akawasalimia na wakati mwingine aliwatania. Siku nyingine alipita akaomba kiti akaketi. Walizungumza hili na lile wakafahamiana. Hatimaye urafiki uliundwa. Kijana yule aliwaambia anafanya kazi kwa mkataba katika shirika moja lisilo la serikali ambalo lilijihusisha na masuala ya tafiti mbalimbali.

Aliwatobolea siri kuwa alikuwa mgeni pale mtaani na jiji la Dar, ingawa alikuwa na shangazi yake aliyeishi Kimara. Nyumbani kwao ni Kilimanjaro na hiyo ilikuwa mara yake kwanza kufika Dar. Aliwaeleza kuwa alikuwa anasubiri majibu ya kidato cha sita. Hakuna siku ambayo dada alifurahi kama hiyo. Alihisi jambo limeongezeka katika nafsi yake. Jambo hilo halikuwepo hapo kabla na sasa limetimiza sehemu ya mwili wake iliyokuwa imekosekana. Alifurahi sana kiasi cha kujikuta akiomba namba ya simu ya yule kijana.

"Naomba namba ya simu kama hutojali," alisema dada kwa aibu za kike. Kitu hicho alikiwaza tu kichwani kwamba atamwomba namba ya simu. Hakudhani kama angepata ujasiri wa kumwomba haraka namna. Alijikuta tu amekwisharopoka. Na neno si kama hela katika mfuko wa shati kwamba ukiitoa kwa bahati mbaya utairudisha. Neno likishatoka kinywani limetoka. Liwe baya au zuri halirudi. Liwe lilitakiwa au halikutakiwa halirudi. Hivyo ilibaki shauri la aliyeambiwa kulikbali au kutolikubali.

"Wala hakuna shida," yule kijana alisema. Aliingiza mkono mfukoni akatoa wallet ambayo alilifungua na kutoa kikadi kidogo. Alimkabidhi. Dada alikipokea akakihifadhi. Kikadi hicho kilikuwa na jina, anuani yake, anuani ya shirika na nafasi yake. Waliagana.

Tukio lile lilimpa kazi kubwa sana dada. Aliihitaji sana namba ya simu ya kijana yule. Hata hivyo hakujua ataanzaje kumpigia au kumtumia ujumbe. Atamwambia nini? Alijiuliza. Ampigie kisha amwambie alikuwa anamsalimia? Halafu baada ya hapo? Kila siku alimsalimia alipowakuta na rafiki yake. Sasa amwambie nini? Hakuwa na jibu. Alibaki nayo ile namba ya simu katika simu yake kama mapambo. Siku zilikimbia na mazoea yaliongezeka baina yao. Japo hakuthubutu kumpigia simu au kumtumia ujumbe.

Siku moja, kama kawaida yao, dada alikutana na rafiki yake katika mkao wao ule wa kila siku. Akili yake ilimtuma kufanya jambo kabla hawajachelewa. Alikwishampenda shida ilikuwa kumwambia. Hivyo, siku hiyo alimwambia rafiki yake ampe mwaliko yule kijana waende sehemu. Rafiki yake hakuvunga. Ilipofika jioni, kama kawaida yule kijana alifika kuwasalimia.

"Samahani! Eti unaweza kupata nafasi siku moja tukatembeatembea?" Rafiki yake dada alimuuliza yule kijana.

"Nafasi yaweza kupatikana. Ulikuwa unapenda iwe lini?" Alijibu kwa upole yule kijana. Kwa jinsi alivyolipokea ombi lile ni kama alilisubiria kwa siku nyingi. Utulivu wake uliongezeka mara dufu.

"Jumamosi au Jumapili," rafiki yake dada alisema.

"Tufanye Jumapili. Leo lini?" Alijibu yule kijana kisha aliuliza.

"Leo ni Jumatano," dada alidakia. Furaha ilikwishakita mizizi moyoni mwake. Mtego ulielekea kunasa windo.

"Basi tufanye Jumapili. Sijui itakuwa saa ngapi?"

"Jioni kama saa kumi hivi. Au pengine uangalie ratiba yako siku hiyo."

"Sawa, haina shida. Angalau mnitembeze kidogo maana mi' mshamba. Napajua ninapoishi na ninapofanya kazi tu," alisema

wakati akisimama. Aliwaaga kisha aliondoka.

*** * ***

Siku ya Jumapili saa kumi yule kijana akiwa amejiandaa kwa mtoko alifika dukani kwa dada. Alivalia suruali ya jeans rangi nyeusi fulana la rangi nyeupe na raba maridadi. Alipofika dukani alimkuta yule rafiki yake dada peke.

“Vipi mbona uko peke yako?” Aliuliza.

“Siye tutangulie yeye atatukuta huko. Anapafahamu,” rafiki yake dada alisema.

“Sawa,” yule kijana alikubali. Waliondoka.

Safari hiyo iliishia sehemu moja si mbali sana na nyumbani. Mahali hapo palikuwa maalumu kwa mapumziko. Paliuzwa vinywaji mbalimbali, vyakula na matunda. Lilikuwa eneo ambalo linavutia kutokana na mandhari yake. Palijengwa midule midogo midogo iliyotosha kwa watu watatu hadi wanne. Watu wengi waliipenda sehemu hiyo kwa kupumzika na kuburudisha akili zao. Mbali na kuuzwa vinywaji na vyakula vya namna mbalimbali, pia palipigwa muziki hasa wa bendi. Utaratibu wake ulikuwa unalipia wakati wa kuingia. Kwa hiyo, walipofika walilipa kisha wakaingia ndani. Walipoingia walitafuta sehemu ambayo palikuwa na viti vitatu kisha waliketi wakamwita muhudumu.

“Mi’ naomba juisi ya matunda,” kijana yule alisema.

“Matunda gani? Tunayo ya mstakaferi, mapera, machungwa na embe!” Akafafanua yule mhudumu.

“Mi’ nipe soda.” Naye rafiki yake dada aliagiza. Mhudumu aliondoka na baada ya kuda kidogo alirejea akiwa na vinywaji alivyoagizwa. Aliweka mezani.

“Ni mahala pazuri sana.”

“Ni kweli pazuri. Ni mara nyingi sana huwa tunapenda kuja hapa siku kama ya leo.”

“Nimepapenda sana. Nitaanza kuja kila Jumapili.”

“Ha ha ha aha ha ha!” Walizungumza huku wakimsubiri dada.

Nusu saa baadaye dada aliwasili akiwa amependeza sana. Alipoingia ndani alikwenda moja kwa moja hadi walipokuwa yule kijana na rafiki yake. Kabla hajakaa alikutana na swali kutoka kwa yule kijana.

“Umependeza sana, lakini mbona umekuja peke yako?” Lilikuwa swali la utani. Dada alikasirika sana. Alikuwa kama mbogo aliyejeruhiwa.

“Umesemaje?” Aliuliza dada kwa sauti iliyoonesha hasira za waziwazi.

“Mbona umekuja peke yako? Siye tuko wawili hapa.” Bila kufahamu yule kijana alilirudia swali lake la utani. Dada alikereka mno. Kisha kama umeme aliikwapua glasi ya juisi ambayo ilinywewa nusu akammwagia yule kijana kwenye t-shirt yake. Kilikuwa kitendo cha muda mfupi sana. Kila mtu alishtuka.

“Akha! We vipi? Ndiyo nini sasa unafanya?” Rafiki yake alimwuliza kwa hasira. Yule kijana aliduwaa asijue imekuwaje. Kumuuliza tu kuwa mbona amekuja peke yake ndiyo imekuwa hivi au kuna sababu nyingine? Alijiuliza. Alimmwangalia dada kwa hasira. Alikasirika sana japo hakusema kitu. Kisha taratibu alisimama akatembea kutoka eneo lile. Dada na rafiki yake walimsindikiza kwa macho. Yule kijana alitokomea kabisa.
Huku nyuma, mara tu baada ya yule kijana kuondoka, dada alianza kutetemeka halafu akaangua kilio. Hakujua kitu gani hasa kilipelekea akachukua uamuzi ule wa kipumbavu. Hakufahamu hasira zile zilitokana kweli na kuulizwa swali lile au kulikuwa na kitu kingine ndani yake. Alijua leo ndiyo ulikuwa mwisho wa mazoea yao na yawezekana pia kutokana na kitendo kile akabadili njia.

Alijuta sana. Alitamani amkimbilie amuombe radhi, lakini alishindwa. Ataanzaje? Alijilaumu kwa kuharibu mwishoni mpango aliousuka. Alikuwa kama mwindaji aliyekaribia kulinasa windo lake lakini kabla hajatupa mshale kuelekea windo hilo alilishtua windo likakimbia. Alilia sana. Siku iliyofuata, walikuwa na mategemeo makubwa ya kumuona yule kijana ili wamuombe radhi kwa kilichotokea jana. Mambo hayakuwa kama walivyodhani. Siku hiyo ilipita bila kumuona wala kuona dalili yake. Nyoyo zao ziliingia simanzi huku dada akijilaumu sana kwa kitendo chake cha jana.

***ITAENDELEA….***

# MIAMBA WA AFRIKA

## Samora Machel - 01

**HISTORIA YA AWALI**

SAMORA Machel alizaliwa katika kijiji cha Madragoa, kwa sasa kinaitwa Chilembene katika Mkoa wa Gaza, nchini Msumbiji. Samola alizaliwa katika familia ya kawaida ya wakulima. Babu yake alikuwa madau mkubwa Gungunhana. Chini ya utawala wa Ureno, baba yake, kama Wamsumbiji wengi weusi, alijulikana kwa jina la kudhalilisha 'indígena' (asili). Yeye kama wengine, alilazimika kukubali kuuza mazao yake kwa bei ya chini kuliko ile ya wakulima wa Kizungu. Pia alilazimishwa kulima pamba inayohitaji nguvu kazi kubwa, ambayo ilichukua muda mrefu kuingia sokoni tofauti na mazao ya chakula yaliyohitajika kwa familia yake. Zaidi ya hapo alikatazwa kuweka alama juu ya mifugo yake ili kuzuia wizi.



Hata hivyo, baba yake Machel alikuwa mkulima mwenye mafanikio. Kufikia mwaka 1940 Alikuwa na majembe manne na ng'ombe 400. Machel alikulia katika kijiji hiki cha wakulima na alisoma shule ya msingi ya misheni. Mnamo 1942, alipelekwa shule nyingine katika mji wa Zonguene Mkoani Gaza. Shule hiyo iliendeshwa na Wamisionari Wakatoliki ambao waliwafundisha watoto kwa lugha na utamaduni wa Kireno. Ingawa alikuwa amemaliza darasa la nne, Machel hakumaliza elimu yake ya sekondari. Hata hivyo, alikuwa na cheti cha sharti la kupata mafunzo ya uuguzi popote nchini Ureno wakati huo, kwa kuwa shule za uuguzi hazikuwa taasisi zinazotoa shahada.

Machel alianza kusomea uuguzi katika mji mkuu wa Lourenço Marques au Maputo ya sasa, kuanzia mwaka 1954. Katika miaka 1950, aliona sehemu ya ardhi yenye rutuba karibu na jamii yake ya wakulima kwenye mto Limpopo ikimilikiwa na serikali ya mkoa na kufanyiwa kazi na walowezi wa Kizungu ambao walitengeneza kwa kanda miundombinu mbalimbali, mipya. Kama wananchi wengine wengi wa Msumbiji waliokuwa wakiishi karibu na mpaka wa Kusini mwa nchi hiyo, baadhi ya jamaa zake walikwenda kufanya kazi katika migodi ya Afrika Kusini ambako nafasi za kazi zilipatikana. Muda mfupi baadaye, mmoja wa kaka zake alikufa katika ajali wakati wa uchimbaji madini. Machel hakuweza kumaliza mafunzo yake katika Hospitali ya Miguel Bombarda huko Lourenço Marques, badala yake alipata nafasi ya kufanya kazi kama msaidizi katika hospitali hiyo hiyo na akapata pesa za kutosha kuendelea na program za masomo ya jioni. Alifanya kazi katika hospitali hiyo hadi alipoondoka na kujiunga na wapigania uhuru wa Msumbiji nchini Tanzania.Vita vya Uhuru wa Msumbiji

MACHEL alivutiwa na itikadi za kupinga ukoloni na alianza shughuli zake za kisiasa katika Hospitali ya Miguel Bombarda huko Lourenço Marques au Maputo ya sasa, ambapo alipinga ujira wa wauguzi weusi kuwa chini kuliko ule wa Wazungu ilhali kazi wanayofanya ni sawa. Mpiganaji Mzungu wa kifashisti, João Ferreira, aliyekuwa mtaalamu wa dawa katika hospitali hiyo, alimpa siri Machel kuwa alikuwa akifuatiliwa PIDE, yaani polisi wa kisiasa wa Ureno. Machel akaondoka Lourenço Marques, mara baada ya ujumbe huo kumfikia. Aliondoka na kufanikiwa kuvuka mpaka na kuingia nchini Afrika Kusini, Swaziland mpaka Botswana. Akiwa Botswana, aliomba lifti kwenye ndege ya Afrika Kusini iliyobeba wanajeshi wa African National Congress waliokuwa wakienda Tanzania. Kamanda wa ANC, J.B. Marks alivutiwa na kijana huyo wa Msumbiji. (kulingana na Joe Slovo) Akaamuwa kumwondoa mmoja wa waajiriwa wa ANC kwenye ndege ili kumwacha Samora Machel apate usafiri. Machel akasafiri kwa ndege hiyo mpaka Tanzania na kujiunga na wapiganaji wa FRELIMO waliokuwapo jijini Dar es Salaam.

***ITAENDELEA...***

# ZAMIRA SANGUTI: ... MAHUSIANO YAKE NA VITABU (Marudio)

**Na Richard Mwambe**

Mwezi huu wa Septemba, Ngurumo ya Mwandishi limefikia Dar es salaam, mpaka Kinondoni Morocco, Mtaa wa Nguchiro, Blok 43. Hapa kuna duka maarufu sana la kuuza vitabu kinajulikana kama Kona ya Riwaya.

Naingia hapa napokelewa na mwanadada mcheshi aliyejisitiri vyema na hijab hata unywele wake mmoja hauonekani.

Ni moja ya  safari ndefu za jarida hili ambazo kwazo twakutana na wadau mbalimbali wa fasihi.

Nani asiyelijua hili duka, nje ya wapenzi wa vitabu vya riwaya waishio jijini Dar es salaam na miji ya kando yake?

Nimemkuta hapa ndani ya duka dogo lililosheheni mawazo lukuki na hadhimu yaliyowekwa kwenye vitabu. Nachelea kusema kwamba, huyu mwanadada mrembo na hivi vitabu wanafanana.

Nimejibanabana hapa dukani, sakafu na kuta za chumba hiki zimejaa vitabu, loh!

Kabla hata sijamwambia aseme nanyi, akaanza kunisimulia visa na mikasa kwa asilimia zaidi ya themanini ya vitabu vilivyopo humu ndani. Ana kipaji cha pekee!

Nimemkatisha hasiendelee kunisimulia ili aongee nanyi kidogo.

Hebu tuambie wewe ni nani na maisha yako kwa kifupi...

Mimi naitwa Zamira  Sanguti ni mzaliwa wa Tanga. Kwenye familia yetu, mimi ni mtoto wa tatu kati ya watoto tisa.

Nilikuwa napenda sana kuwa mwanariadha, lakini baba yangu alikua hataki hata kusikia nacheza michezo hiyo. Kwa kuwa nilikua naongoza katika kikundi chetu nikawa namchukia sana baba.

Tofauti na mama, yeye alikuwa hana shida kwakuwa alikuwa mwalimu na alikuwa akinisapoti. Baba alipokuja kujua hivyo, akaenda hadi shule niliyokua nikisoma akawaambia kanipeleka pale nisome sio kukimbia kimbia. Basi, nikatolewa kwenye ule mchezo. kwakweli niliumia sana nikazidisha chuki kwa baba sitakuja kusahau

Kwanini umejenga mahusiano makubwa na vitabu?
Napenda kusoma vitabu kwanza mi sina rafiki, sina mpenzi. Rafiki na mpenzi wangu ni vitabu na nikikosa kitabu naumwa.

Hapa uliponikuta nauza vitabu, napenda kufanya kazi ya kuuza vitabu kwa sababu  napenda vitabu..

Waandishi wengi wanalalamika kuwa vitabu havina soko, wewe kama muuzaji unalizungumziaje hilo?

Soko la vitabu ni kubwa hapa nchini kuliko mnavyofikiria. Watu wanapenda kusoma vitabu haswa mikoani.

Amini usiamini, wasomaji wengi wa vitabu ni wamama na wadada wanaobaki nyumbani. Kiukweli tunahitaji kazi mpya. Wandishi acheni uvivu

Hebu waambie neno waandishi wakusikie, ongeza sauti wasikie vizuri

Wandishi wa vitabu nawambia zipendeni kazi zenu na msiogope wa somaji pale wanapo taka kujua visa vya vitabu vyenu. Wengi wenu hampendi kuulizwa maswali tena mnachukia. Mimi mmojawapo, napenda kuwauliza maswali waandishi, lakini wengi wananichukia kwa kuwaulizauliza.

Kama upo nje ya Dar, Unaweza kuagiza kitabu na Zamira atakutumia bila wasiwasi. Ni mwaminifu sana. Basi wasiliana naye kwa 0655428085 (kwa ajili ya manunuzi ya vitabu tu!)



# MPIGA MBIO — 17



Richard Mwambe

*Ilipoishia...*

**"Maana siku ile umekuja 'dada nisaidie hii cheki' nikajua mmm hapa kuna jambo tangu lini Ikunda na misaada ya watu. Waswahili husema pafukapo moshi jua pana moto," Prisca akaongea kwa furaha huku akiiacha barabara kuu na kuingia kwenye supermarket kubwa ya kisasa iliyojengwa maeneo ya Mwenge.**

*Endelea...*

"Sasa Iku' tufanye manunuzi hapa halafu tupite mahali tumsalimie rafiki yangu kisha nikurudishe, asije shem kufika we haupo!" akaongea huku akifunga lile gari. Ndani ya supermarket hiyo, walichukua nusu saa tu. Na safari ya pili ilianza.

"Tunaelekea wapi?" Ikunda akauliza huku kila wakati akiiangalia simu yake.
"Tutasimama Mwenge kidogo kuna jamaa namcheki kisha tunarudi," Prisca akamwambia Ikunda.

"Haina neno, tusichelewe tu!" Ikunda akasisitiza. Hao! Wakaondoka mpaka Baa ya Sokoni ambako Habib alikuwa akiwasubiri.
Baa ya Sokoni ilikuwa maarufu sana katika eneo hilo. Ilijengwa kisasa sana, yenye muziki mzito, eneo la wanywaji wa kawaida na wale VIP yalitengwa. Baa hiyo, upande wa nyuma ilikuwa imeunganishwa na loji kubwa kwa ajili ya wageni wanaopenda kuishi hapo kwa muda. Ukiwa kwenye loji hiyo huwezi kabisa kusikia yanayoendelea huko baa. Ilikuwa kimya, tulivu, safi na nzuri.

Prisca alimshawishi Ikunda kuteremka waingie ndani ya baa hiyo kwa dakika chache. Ilikuwa ngumu. Ikunda hakuzoea kabisa kuingia maeneo hayo, aliogopa. Baada ya dakika kumi za kuhoji na kujibiwa huku akihakikishiwa usalama wake dhidi ya walevi wenye uchu, alikubali shingo upande. Wakavuta hatua na kuelekea huko VIP huku Ikunda akigeuka nyuma mara kwa mara.

*** *** ***

Baada ya kuchomoka pale Mwananyamala Inn, Kenny aliona mambo si mambo. Nyuma tu ya eneo lile kulikuwa na taksi. Akaidaka moja kumwambia dereva amkimbize Magomeni haraka. Yule dereva akapita mbele ya lile eneo na Kenny aliwaona wale askari wakiwa nje na yule mwanamke wa Kiarabu.

"Magomeni ipi bro'?" yule dereva akauliza.

"Magomeni Kanisani!" akajibu. Yule dereva akakanyaga mafuta na kuongeza kasi mpaka eneo aliloambiwa. Akaegesha gari mbele ya Kanisa la Mashahidi wa Uganda. Akamlipa yule dereva ujira wake na kumwacha aende. Alipohakikisha ameshatoweka, naye akapotelea mitaani kuelekea Mapipa. Àkiwa njiani, akainua simu yake nà kumpigia Ikunda.

"Mambo vipi mtoto mzuri?" akamsabahi.
"Safi, uko wapi mpenzi?" Ikunda akajibu.
"Nipo maeneo ya Kariakoo kuna jamaa zangu nakutana nao halafu nakuja kwako…"
"Sawa mpenzi… ila nimetoka kidogo na da' Prisca wa kazini, nitawahi kurudi sichelewi…"
"Sawa, fanya hivyo, nitakupigia wakati natoka huku!"
Wapenzi hao wakakubaliana, simu ikakatwa. Kenny akaongeza kasi mpaka Magomeni Mapipa na kuingia nyumba ileile aliyoingia Kebby. Wakakutana!

*** *** ***

Mara tu Ikunda alipokata simu, akaingia kwenye kile chumba cha VIP pamoja na Prisca. Rangi za taa ndani ya chumba hicho, zilifanya kila kitu kibadili mwonekano wake. Ikunda akasimama kama dakika nzima ili macho yake yazoee ile mianga. Kisha akamfuata Prisca kule anakoelekea.

Habibu aliwaona tangu wanavyoingia. Akajiramba papi za midomo yake kwa uchu. Akaingiza mkono mfukoni na kupapasa kama pakiti yake ya dawa ipo. Ipo! Akatikisa kichwa juu chini na kusimama pindi walipokaribia. Habibu akamkumbatia Prisca na kumpiga mabusu yaliyojawa mahaba mazito.

Ikunda alipomwona Habibu alitamani ageuze na kurudi alikotoka. Miguu ilimwingia ganzi, hakuelewa nini kinaendelea. Hakumpenda mwanaume huyo

# MPIGA MBIO — 17



seuze kuwa naye karibu! Alipoona Habibu akimpa Prisca kumbatio lile lililojaa huba, moyo ukamtulia. *Kumbe P' na Habibu wapenzi!* Akawaza. Laiti angelijua ghiliba inayofànyika, hasingewaza hayo yanayomfariji. Wakaketi na kuagiziwa vinywaji. Ikunda aliagiza sharubati ya embe baada ya kushinda ushawishi wa wawili hao wa kunywa pombe.

*** *** ***

Prisca na Habibu walikuwa na mazungumzo marefu yaliyojawa visa na mikasa ya maisha. Ikunda alibaki kimya akiwasikiliza. Akili yake wala haikuwa pale. Aliendelea kunywa sharubati yake taratibu huku akiangalia saa Kila wakati. Muda uliyoyoma, nusu saa ya Prisca ikawa saa nzima na zaidi. Moyoni na mawazoni mwa Ikunda alijaa Kenneth tu. Mara zote alikwepesha macho yake Kila yalipotaka kugongana na ya Habibu.

Prisca alijua na alifanya makusudi kumleta Ikunda mahali hapo. Habibu bado alikuwa anatafuta nafasi ya kufanya alilolitaka, lakini nafasi ilikuwa ngumu.
"Samahani, P' chooni wapi?" Ikunda akamuuliza mwanamke mwenzake.

*Bingo!* Habibu alijisemea moyoni. Kijana huyu alikuwa akisubiri sentensi hiyo kwa hamu zote. Prisca naye alijua tayari mchezo unaingia mahali pake. Prisca alitamani Ikunda afanywe kilichopangwa kumkomoa kwa sababu tu amemnasa Kenneth ambaye hata yeye alimhusudu.

“Ngoja nikusindikize shoga, wasije kukuiba bure nikalaumiwa!” Prisca alijishauwa, akainuka na kumpeleka Ikunda msalani. Haukuwa msaada Bali kupoteza ushahidi kwa litalotokea. Alijua anachokifanya. Alikusudia.

Dakika tano tu, Prisca na Ikunda walirudi. Ikunda alimlalamikia shogaye juu ya muda, akatamani aondokee hukohuko msalani lakini Prisca alimsihi kumsubiri amalizie bia yake. Ikawa hivyo.
Huku nyuma, Habibu, kwa kasi ya ajabu, aliingiza mkono mfukoni na kutoa kile kijikaratasi chake. Akakung'utia ungaunga uliokuwa humo kwenye bilauri aliyokuwa akiitumia Ikunda. Kisha akatoa cheko la moyoni, cheko la ushindi. Akaketi vizuri. *Kazi imeisha!* Akajiwazia. Warembo wale walirudi, na Prisca akawa wa kwanza kupiga mafunda kadhaa ya bia yake. Ikunda naye akafanya vivyo hivyo.

Dakika kumi zilizofuata, alijihisi vibaya. Alihisi macho mazito, nguvu zikimpotea.
“Prisca!” aliita kwa shida. Prisca alimtazama kabla ya kuitikia, “Shoga vipi?” akauliza.
“Najisikia vibaya P…. ” Ikunda alijikuta anashindwa kuendelea kuzungumza. Akainua simu yake kwa shida wakati Prisca akikubaliana jambo na Habibu. Ikunda akafanikiwa kupiga namba ya Kenneth kwa taabu lakini hakuweza kuongea. Mkono wake ulishindwa hata kuipeleka simu ile sikioni.

“Oya mzigo tayari huu…” Prisca akamwambia Habibu.
“Haina shida, niachie mimi, hapa wananifahamu vizuri shughuli zangu…” Habibu akajimbu Prisca.

*** *** ***

“Mmefuata nini na wakati bado?” Mzee Ngoleko akawauliza Kenny na Kebby.
“Mi nimejikuta tu nakuja hapa…” Kenneth akajibu.
“Mi nimeota ndoto mbaya kabisa ndo maana nikaona nije…” Kebby akaeleza.
“Umeota nini eleza!” yule mzee akamwambia Kebby. Kebby hakuwa na namna akasimulia ile ndoto kama ilivyo. Alipomaliza, Mzee Ngoleko akamgeukia Kenny aliyekuwa kapigwa na bumbuwazi.

“Kenneth!” akaita. Naye Kenneth alipogutuka akatazamana na Mzee huyo, “unafanya nini kijana… unavunja kiapo…”… “Hapana mzee!!”
“Hapana nini? Wewe una mwanamke… na nilishawaambia dawa niliyowapa hutakiwi kuwa na mwanamke wa kudumu. Yaani wewe ukiwa na shida zako utafute, umalize, uondoke… usiwekeze!” Ngoleko alikasirika.

“Mzee ni kweli, lakini Mimi sijafanya chochote na huyo mwanamke, na ulituambia kuwa kama mmoja wetu anapata mchumba basi amlete aogeshwe kwanza…” Kenneth akaeleza.
“Naaam!”

***ITAENDELEA***

# SHUBAKA LA VITABU

**SELINA BANZI anatueleza kuhusu Shubaka la vitabu. Ni mahojiano ya kirafiki kati yake na mwandishi wetu. Yeye kama mkufunzi msaidizi bado anathamini vitabu na yaliyomo ndani yake. Ni msomaji mzuri, anayependa kusoma kila wakati. Lakini hivyo avisomavyo uvihifadhi wapi?**

Kwa kuanza, jitambulishe na utueleze kuhusu wewe kwa kifupi… yale majibu yako marefu marefu siyataki, safu hii ni fupi!



Jina langu ni Selina Banzi. Ni mkufunzi msaidizi katika chuo kikuu Cha Dodoma (UDOM). Mimi ni mpenzi wa vitabu vya riwaya hasa za kijasusi/kipelelezi. Nilianza kusoma vitabu hivi nikiwa darasa la tatu. Nakumbuka riwaya niliyoanza nayo inaitwa KIU YA HAKI.

Tangu hapo nimekuwa mfuatiliaji wa riwaya za waandishi wengi kama Richard Mwambe, Japhet Nyang'oro, Patrick C.K., Bahati Mwamba, Abyas Mzigua na wengine wengi.

Asante .... nikuulize swali, tunaposema Shubaka la Vitabu we unaelewa ni kitu Gani?

Ni kifaa/eneo ambalo mtu anatumia kuhifadhia vitabu au nyaraka zingine ni shelf hili.

Ok! Wewe unalo Shubaka la Vitabu?

Ndiyo, ninalo nyumbani… Ofisini ndio Sina ila niko kwa *process* kulipata

Hongera sana! Sasa Tuambie Shubaka lako wewe limebeba vitabu Gani? Yaani maudhui Gani?

Shubaka langu limebeba maudhui ya dini, ujasusi na upelelezi, *diaries* zenye kumbukumbu binafsi, baadhi ya *assignments* na daftari nilizokuwa natumia shuleni

Waoh safi sana... Kwa hiyo mwenyewe unaturingishia Shubaka lako! Sawa. Vitabu unavyosoma vinakusaidiaje kwa kazi uayoifanya?

Kama mwalimu vimenisaidia kujua *psychology* ya wanafunzi na watu mbalimbali, pia vitabu hivi vinakuza sana *reasoning, thinking* na *argumentation* ukiwa msomaji utaona tu mabadiliko ndani Yako.

Vizuri mwalimu... Kweli ukiwa mwalimu lazima usome sana. Hata Mimi ninaamini kuwa mwalimu anajua Kila kitu. Tuambie harakaharaka, una vitabu vingapi?

Mh! Ngoja nikahesabu…

Eh! Kuhesabu tena! Ndo maana ninekwanbia 'haraka haraka' yaani fikiria tu utuambie

Nadhani 80 hiviii

Sasa, kuna desturi ya wasomaji na wapenzi wa vitabu kuuambia uma idadi ya vitabu wanavyosoma kwa mwaka. Je wewe kwa mwaka 2022 umeisoma vitabu vingapi?

Mwaka Jana nimesoma vitabu visivyopungua 20

Hongera sana! La mwisho, unawaambia nini wanaokusoma hapa kuhusu usomaji wa vitabu?

Usomaji wa vitabu ni mzuri sana, kwanza unakuongezea misamiati na ujuzi wa lugha yetu adhimu ya Kiswahili, pili nikupe siri, Mimi ni mmoja wa wasoma masomo kanisani... kutokana na uzoefu wa kusoma vitabu mbalimbali sijawahi tetereka, natamka maneno vizuri bila shida. Alafu Hawa waandishi wanaandika mambo ambayo baadhi yanatokea katika jamii zetu, Kuna *situation* tunapitia vipindi tofauti tofauti Sasa vitabu hivi vinaweza kutusaidia kuhusianisha na maisha yetu ya kila siku. Hivi vitabu vinatupa maarifa mengi sana.

Asante sana. Ngurumo ya Mwandishi tunakutakia usomaji mwema wa vitabu. Ni matumaini yetu kuwa wengi wamejifunza kupitia andiko lako.

# KITABU NILICHOSOMA

## KOVU LA MOYO

***Anaandika Princess Jose***

KOVU LA MOYO....Ni kitabu ambacho nilivutiwa nacho kukisoma pale nilipoona kinaelezewa kinahusu nini na mwandishi Mariam Mbano.. Katika Hadithi zote mbili zilizoandikwa katika kitabu cha KOVU LA MOYO...Hadithi ya getrude na Florida zimenifunza vingi
Baadhi ya vitu ambavyo nimejifunza Ni; Si kila mahusiano ya muda mrefu au mfupi huishia ndoa sababu kuna vingi husababisha safari ya wawili kuishia njiani kama
@ Kutofautiana malengo,
@ Dini/kabila
@ Ugomvi wa mara kwa mara
@ Umbali
Katika Kovu la Moyo
Imeelezea kwa kina sana kila kitu kinachohusu mahusiano na namna bora ya kukabiliana na changamoto hizo....

***Nasra Malik anatueleza***
Nafurahia kumiliki kitabu cha KOVU LA MOYO
Kwenye. kitabu cha KOVU LA MOYO nimejifunza yafuatayo
1) Nimejifunza kuna maisha baada ya kuachana
Mnaweza kuwa mlipendana sana na mkaja kuachana na bado msiwe maadui
3) Nimejifunza kuwa na kipindi cha ukimya
Kipindi hiki cha ukimya kina faida nyingi
a) kujitathimini
b) kujiboresha
c) kujirekebisha
d) kujijenga
4) kimenifunza namna bora ya kukabiliana na changamoto za kuachana
5) Nimejifunza unaweza kurudiana na mwenza wako mlieachana kama tu utaweza kujipa muda kwa mf. Florida alivojipa muda baada ya kuachana na mwenza wake Sweetbert
Kitabu hiki cha KOVU LA MOYO kimegusa maisha yangu ya kila siku kwa kuzidisha subira kwenye baadhi ya mambo sio sawa unapokutwa na changamoto kufanya
a) fujo
b) kulalamika
c) kulaumu
d) kutoa maamuzi ya haraka
kwenye changamoto zinazokukabili

***Aneth Januari Mdotha anaongezea...***
Nimejifunza vingi saana katika kitabu hiki cha Kovu la Moyo, kwanza kabisa nimejifunza namna ya kuishi vizuri na mwenza wako na kuwa na tabia zinazomfurahisha mwenza wako, nimeona tabia za Getrude ambavyo zilikuwa zinamuudhi mwenza wake George.

Pia nimejifunza vile ambavyo wanawake tunaathirika sana na kuvunjika kwa mahusiano, Kingine nilichojifunza ni namna ambavyo unaweza kufanya mkaachana kwa amani bila ugomvi tumeona baada ya ukimya unaweza kutuma sms ya amani kabisa ili maisha mengine yaendelee.


Kingine kikubwa ambacho kimenijenga ni namna ambavyo unaweza kukabiliana na hisia zako unapokuwa na maumivu hii binafsi imenisaidia mno, lakini kingine ni vile kitabu hiki kimeelezea namna ambavyo inawezekana kurudisha hisia zilizokufa na hata mkaweza kurudiana na kuwa imara zaidi. Kwakweli kitabu kimegusa maeneo muhimu sana.

Asante Mwandishi wa kitabu Mariam Mbano

***Anaandika Happiness Joseph***
Kupitia kitabu hiki nimejifunza mambo mbalimbali juu ya uhusiano/mahusiano, Tiririka Pamoja Nami

a. Nimejifunza kwamba Kila jambo ni swala la muda tu, nmeona jinsi masaibu yaliyomkuta Getu kuhusu George na Beatrice, ndio Yale Yale yalomkuta Mama Temba lakini baadaye (baada ya muda) Ma Temba alimpata Baba Temba na Mahaba yakawa motomotooooo

b. Nimejifunza kufikiri kabla ya kutenda,maamuzi ya Sasa ni matokeo ya baadae, nimeona jinsi Getu baada ya hekahekaa za kumkomoa George kupitia Beatrice hakupata faida yoyote badala yake aliambulia patupu mwishowe AKAKATA SHAURI(UK 13)
c. Nimejifunza kuukubali ukweli na kusonga mbele, haijalishi mahusiano yana miaka afu tatu au la, haijalishi nimemlipia au kanilipia ada, haijalishi nini wala nini, mahusiano yakigonga mwamba ni kukubali tu yamefika mwisho yaani nimeachwa au nimeacha Haina mbambambaa .



# Tangazo

**Ile App ya Jamvi la Simulizi uliyokuwa ukiisubiri kwa hamu sasa ipo tayari, ipo Playstore kwa wale wote watumiaji wa Android. Ipakue sasa ujisomee riwaya ya Kamanda Amata bure, majarida ya Ngurumo ya Mwandishi matoleo yote na picha za matukio mbalimbali. Kwanini ujitenge? Jiunge na familia kubwa ya Jamvi la Simulizi.**

**Jinsi ya kufanya:-**

**Fungua simu yako, chagua Play Store > kwenye search andika 'Jamvi la Simulizi'> kisha bofya Download/Install > Open**

**Ikishafunguka basi ingiza email yako na password… tayari utakuwa umejiunga. Njoo tufurahi pamoja.**










---

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com